



UFANISI WA DAWA

Uavyaji mimba kwa kutumia Mifepristone pamoja na Misoprostol ni salama sana na ni bora kwa asilimia tisini na tano hadi tisini na nane (95-98%) mara nydingi, kutamatisha mimba bila haja ya matibabu ya ziada kwa wakati wa wiki kumi za kwanza za mimba

IKIWA DAWA HAZIKUFANYA KAZI



Rudia uavyaji mimba kwa kutumia mifepristone na misoprostol tena au tumia njia ya MVA.

Kuna hatari ndogo sana ya kasoro za uzazi ikiwa mimba itaendelea kukua baada ya kutumia misoprostol.



JE, UAVYAJI MIMBA ULIKUWA KAMILIFU?

Hata kama mwanamke anahisi kwamba ujauzito ule ultamatika, ni muhimu kuhakikisha kuwa uavyaji mimba umekamilika. Wanawake wanapaswa kufanya ultrasound baada ya siku kumi baada ya kuavyia mimba kwa kutumia mifepristone na misoprostol au kupima ujauzito wiki tatu hadi wiki nne baada ya kuavya mimba.



BAADA YA KUAVYIA MIMBA

Baada ya utoaji mimba, mwanamke anapaswa kutarajia kutokwa na damu kwa wiki ya kwanza hadi ya tatu, lakini kila mwanamke ni tofauti. Baadaye, mwanamke anapaswa kuthibitisha kwamba uavyaji wa mimba umekamilika.

Wanawake wanashauriwa kutoingiza chochote ndani ya uke wao wala wasifanye ngono mpaka damu nydingi iwache kutoka kwenye uke wake kwa muda wa kama siku mbili, baada ya uavyaji wa mimba.

Mwanamke anaweza kupata mimba mara tu baada ya kuavya mimba!

Ikiwa hataki kupata mimba kwa haraka, anaweza kuanza kupanga uzazi kuzuia mimba nydingine isiyotarajiwa.



CONTACTS

Women Help Women

WEB: [HTTPS://WOMENHELP.ORG/](https://WOMENHELP.ORG/)

EMAIL: INFO@WOMENHELP.ORG

TWITTER: @WOMENHELPORG

FACEBOOK: WOMENHELPWOMENINTERNATIONAL


MAMA Network: Mobilizing Activists around Medical Abortion (MAMA).
WEB: WWW.MAMANETWORK.ORG

UAVYAJI MIMBA

NA MIFEPRISTONE

PAMOJA NA MISOPROSTOL

(JINSI YA KUTUMIA
HIZI DAWA MBILI PAMOJA)





Jinsi inavyofanyaje kazi

Uavyaji wa mimba kwa kutumia dawa, husababisha mchakato kama wa mimba kuperomoka yenye



Mifepristone huzua progestrone, homoni muhimu ili kudumisha ujauzito na pia hufanya uterasi kukubali Misoprostol.



Misoprostol husababisha vipunguo vya uzazi, ambayo husababisha tishu za ujauzito kusukumwa nje, vifungo vya damu viliyoshikana na pia damu.

LINI MISOPROSTOL NA MIFEPRISTONE ZAWEZA TUMIKA KWA KUAVYA MIMBA KWA NJIA YA USALAMA?



Hasa katika wiki kumi za kwanza za kuhesabu ujauzito kutoka siku ya kwanza ya mzunguko wa hedhi ya mwisho



JINSI GANI INAWEZATUMIKA KWA KUAVYA MIMBA KWA NJIA SALAMA?



Mwanamke atahitaji kidonge kimoja cha Mifepristone (200 mg) pamoja na vidonge vine vya Misoprostol (200 mcg kila moja)



Kidonge kimoja cha **mifepristone** (200mg) kinapaswa kumezwu na glasi ya maji

Baada ya masaa ishirini na nne wanamke anapaswa **kuweka vidonge vinne (200mg kila moja) vya misoprostol**



katikati ya gamu na shavu, mbili upande wa kushoto na mbili upande wa kulia au chini ya ulimi.

Dawa zote nne (misoprostol) zapaswa kuachwa ndani ya mdomo kwa muda wa dakika thelathini hadi ziyeuke.



MADHARA INAYOWEZA KUONEKANA

Ndani ya masaa ishirini na nne, dalili zifuatazo zinaweza kutokea: kichefuchefu, kutapika, kuharisha, kupatwa na joto bila baridi au na baridi, maumivu ya kichwa au kizunguzungu. Madhara haya sio hatari na yataweka baada ya masaa machache.



NINI INATARAJIKA BAADA YA KUTUMIA DAWA?



Maumivu na kutokwa damu Zaidi kuliko inavyotakikana wakati wa hedhi.



Kwa kesi asilimia tisini, mimba huweza kutoka wakati wa masaa ishirini na nne ya kwanza.



Kulingana na urefu wa muda ambaa mwanamke amekuwa na ujauzito, kuna uwezekano atatokwa na damu nyingi zaidi au maumivu yatakuwa makali.



Anaweza kutumia **ibuprofen au panadol** ili kupunguza maumivu.



ISHARA ZA ONYO WAKATI WA MATATIZO NI ZIPI?



Kutokwa na damu nyngi (kutumia padi mbili au tatu zilizo jaa damu kwa kipindi cha lisaa limoja kwa muda wa masaa mawili au matatu mfululizo)



Kupatwa na joto ya mwili Zaidi ya celcius thelathini na tisa au thelathini na nane zaidi ya masaa ishirini na nne.



Maumivu makali ambayo hayaondoki hata baada ya kutumia dawa za kutuliza maumivu siku chache baada ya kutumia dawa za kuavya mimba.



Kutokwa na uchafu wenye harufu mbaya kwenye uke

NINI CHA KUFANYA WAKATI UNATATIZO?



Nenda mara moja kwenye kituo cha afya.

Katika hali ya dharura ya matibabu, wahudumu wa afya wana wajibu wa kuhudhuria mtu yule kwa haraka. Matibabu ya matatizo baada ya kutumia mifepristone na misoprostol ni sawa na matibabu ya matatizo baada ya mimba kuperomoka yenye. Haiwezekani kuona tofauti kati ya mimba iliyo poromoka yenye na uavyaji wa mimba ikitumia mifepristone na misoprostol. Mwanamke anayehitaji msaada wa matibabu anaweza kusema ya kwamba mimba imeporomoka yenye.

